***KUMB: PPR/19 - 09/1***

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 4 SEPTEMBA 2019**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 4 Septemba 2019.** Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

(a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya **Dar es Salaam**, zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 7 Agosti 2019. Kwa mwezi Septemba 2019, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 83/lita (sawa na asilimia 3.87), Shilingi 61/lita (sawa na asilimia 2.90) na Shilingi 46/lita (sawa na asilimia 2.22), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 82.96/lita (sawa na asilimia 4.09) na Shilingi 60.95/lita (sawa na asilimia 3.07) na Shilingi 46.12/lita (sawa na asilimia 2.35), mtawalia.

(b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya **Tanga** nazo zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 7 Agosti 2019. Kwa mwezi Septemba 2019, bei za rejareja za Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kaskazini** (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara) zimeongezeka kwa Shilingi 108/lita (sawa na asilimia 4.95) na Shilingi 72/lita (sawa na asilimia 3.36), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 108.04/lita (sawa na asilimia 5.23) na Shilingi 71.41/lita (sawa na asilimia 3.56), mtawalia. *Bei za Mafuta ya Taa kwa Mikoa ya Kaskazini zitaendelea kuwa bei zile zilizochapishwa tarehe 7 Agosti 2019 kwa sababu hakuna shehena ya bidhaa hiyo iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Tanga kwa mwezi wa Agosti 2019*.

(c) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya **Mtwara** zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 3 Julai 2019. Kwa mwezi Agosti 2019, bei za rejareja za Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kusini** (Lindi, Mtwara na Ruvuma) zimeongezeka kwa Shilingi 99/lita (sawa na asilimia 4.48) na Shilingi 62/lita (sawa na asilimia 2.85), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa Shilingi 99.09/lita (sawa na asilimia 4.73) na Shilingi 61.41/lita (sawa na asilimia 3.02), mtawalia. Aidha, kwa kuwa hakuna Mafuta ya Taa yaliyopokelewa katika bandari ya Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa tajwa wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa mikoa hiyo zinatokana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika.

(d) Kwa kiasi kikubwa, ongezeko la bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara linatokana na kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la dunia na mabadiliko ya gharama za usafirishaji (*BPS premiums*) kama inavyoonekana katika **Jedwali C**.

(e) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

(f) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

(g) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*)** kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula)* iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 163 la mwezi Aprili 2018 na Gazeti la Serikali Na. 269 la mwezi Juni 2018**.

(h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**

(i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

## JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA

| **Mji** | **Bei Kikomo** | | |
|---|---|---|---|
| | **Petroli (Shs/Lita)** | **Dizeli (Shs/Lita)** | **Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)** |
| **Dar es Salaam** | **2,236** | **2,168** | **2,132** |
| **Arusha** | **2,356** | **2,259** | **2,123** |
| Arumeru (Usa West) | 2,356 | 2,259 | 2,123 |
| Karatu | 2,375 | 2,278 | 2,141 |
| Longido | 2,367 | 2,270 | 2,134 |
| Monduli | 2,362 | 2,265 | 2,129 |
| Monduli-Makuyuni | 2,366 | 2,269 | 2,133 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 2,441 | 2,344 | 2,208 |
| **Pwani (Kibaha)** | **2,240** | **2,173** | **2,137** |
| Bagamoyo | 2,247 | 2,179 | 2,143 |
| Chalinze Junction | 2,250 | 2,182 | 2,147 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Chalinze (Msata) | 2,254 | 2,187 | 2,151 |
| Kibiti | 2,256 | 2,189 | 2,153 |
| Kisarawe | 2,243 | 2,175 | 2,139 |
| Mkuranga | 2,246 | 2,178 | 2,142 |
| Rufiji | 2,264 | 2,196 | 2,160 |
| **Dodoma** | **2,295** | **2,227** | **2,191** |
| Bahi | 2,302 | 2,234 | 2,198 |
| Chamwino | 2,290 | 2,222 | 2,186 |
| Chemba | 2,321 | 2,254 | 2,218 |
| Kondoa | 2,328 | 2,260 | 2,224 |
| Kongwa | 2,292 | 2,224 | 2,188 |
| Mpwapwa | 2,296 | 2,228 | 2,192 |
| Mtera (Makatopora) | 2,314 | 2,246 | 2,210 |
| **Geita** | **2,401** | **2,334** | **2,298** |
| Bukombe | 2,390 | 2,323 | 2,287 |
| Chato | 2,422 | 2,355 | 2,319 |
| Mbogwe | 2,439 | 2,372 | 2,336 |
| Nyang'hwale | 2,416 | 2,349 | 2,313 |
| **Iringa** | **2,300** | **2,232** | **2,196** |
| Ismani | 2,305 | 2,238 | 2,202 |
| Kilolo | 2,304 | 2,237 | 2,201 |
| Mufindi (Mafinga) | 2,310 | 2,242 | 2,207 |
| **Kagera (Bukoba)** | **2,451** | **2,384** | **2,348** |
| Biharamulo | 2,426 | 2,358 | 2,322 |
| Karagwe (Kayanga) | 2,468 | 2,400 | 2,364 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 2,474 | 2,406 | 2,370 |
| Muleba | 2,451 | 2,384 | 2,348 |
| Ngara | 2,439 | 2,372 | 2,336 |
| Misenyi | 2,460 | 2,392 | 2,356 |
| **Katavi (Mpanda)** | 2,444 | 2,376 | 2,340 |
| Mlele (Inyonga) | 2,426 | 2,358 | 2,322 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 2,436 | 2,369 | 2,333 |
| **Kigoma** | **2,467** | **2,400** | **2,364** |
| Uvinza (Lugufu) | 2,480 | 2,412 | 2,376 |
| Buhigwe | 2,457 | 2,389 | 2,353 |
| Kakonko | 2,424 | 2,357 | 2,321 |
| Kasulu | 2,453 | 2,386 | 2,350 |
| Kibondo | 2,432 | 2,364 | 2,328 |
| **Kilimanjaro (Moshi)** | **2,346** | **2,249** | **2,113** |
| Hai (Bomang'ombe) | 2,349 | 2,252 | 2,116 |
| Mwanga | 2,339 | 2,242 | 2,106 |
| Rombo (Mkuu) | 2,363 | 2,266 | 2,129 |
| Same | 2,332 | 2,235 | 2,099 |
| Siha (Sanya Juu) | 2,352 | 2,255 | 2,119 |
| **Lindi** | **2,331** | **2,236** | **2,191** |
| Lindi-Mtama | 2,336 | 2,240 | 2,209 |
| Kilwa Masoko | 2,355 | 2,260 | 2,166 |
| Liwale | 2,367 | 2,271 | 2,212 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Nachingwea | 2,351 | 2,256 | 2,220 |
| Ruangwa | 2,357 | 2,262 | 2,222 |
| **Manyara (Babati)** | **2,390** | **2,293** | **2,157** |
| Hanang (Katesh) | 2,401 | 2,304 | 2,168 |
| Kiteto (Kibaya) | 2,406 | 2,309 | 2,172 |
| Mbulu | 2,403 | 2,306 | 2,170 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 2,422 | 2,325 | 2,189 |
| **Mara (Musoma)** | **2,415** | **2,347** | **2,311** |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 2,455 | 2,388 | 2,352 |
| Rorya (Ingirijuu) | 2,423 | 2,356 | 2,320 |
| Rorya (Shirati) | 2,458 | 2,391 | 2,355 |
| Bunda | 2,406 | 2,338 | 2,302 |
| Bunda (Kisorya) | 2,415 | 2,348 | 2,312 |
| Butiama | 2,411 | 2,344 | 2,308 |
| Serengeti (Mugumu) | 2,460 | 2,393 | 2,357 |
| Tarime | 2,426 | 2,358 | 2,322 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 2,430 | 2,363 | 2,327 |
| **Mbeya** | **2,343** | **2,275** | **2,239** |
| Chunya | 2,353 | 2,285 | 2,249 |
| Chunya (Makongolosi) | 2,367 | 2,299 | 2,263 |
| Kyela | 2,359 | 2,291 | 2,255 |
| Mbarali (Rujewa) | 2,327 | 2,260 | 2,224 |
| Rungwe (Tukuyu) | 2,352 | 2,284 | 2,248 |
| **Morogoro** | **2,261** | **2,193** | **2,157** |
| Mikumi | 2,277 | 2,209 | 2,173 |
| Kilombero (Ifakara) | 2,299 | 2,231 | 2,195 |
| Kilombero (Mlimba) | 2,321 | 2,254 | 2,218 |
| Kilombero (Mngeta) | 2,310 | 2,243 | 2,207 |
| Ulanga (Mahenge) | 2,309 | 2,242 | 2,206 |
| Malinyi | 2,320 | 2,252 | 2,216 |
| Kilosa | 2,279 | 2,212 | 2,176 |
| Gairo | 2,279 | 2,212 | 2,176 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 2,271 | 2,204 | 2,168 |
| Mvomero (Sanga Sanga) | 2,261 | 2,193 | 2,157 |
| Turiani | 2,286 | 2,218 | 2,182 |
| **Mtwara** | **2,317** | **2,222** | **2,205** |
| Nanyumbu (Mangaka) | 2,354 | 2,258 | 2,254 |
| Masasi | 2,334 | 2,238 | 2,230 |
| Newala | 2,338 | 2,243 | 2,237 |
| Tandahimba | 2,331 | 2,236 | 2,230 |
| Nanyamba | 2,331 | 2,236 | 2,230 |
| **Mwanza** | **2,386** | **2,318** | **2,283** |
| Kwimba | 2,404 | 2,336 | 2,300 |
| Magu | 2,394 | 2,327 | 2,291 |
| Misungwi | 2,380 | 2,313 | 2,277 |
| Sengerema | 2,419 | 2,351 | 2,315 |
| Ukerewe | 2,446 | 2,378 | 2,342 |
| **Njombe** | **2,328** | **2,261** | **2,225** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Njombe (Kidegembye) | 2,349 | 2,281 | 2,245 |
| Ludewa | 2,366 | 2,299 | 2,263 |
| Makambako | 2,321 | 2,253 | 2,217 |
| Makete | 2,359 | 2,292 | 2,256 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 2,326 | 2,259 | 2,223 |
| **Rukwa (Sumbawanga)** | **2,409** | **2,341** | **2,305** |
| Sumbawanga Rural (Mtowisa) | 2,409 | 2,341 | 2,305 |
| Kalambo (Matai) | 2,416 | 2,348 | 2,313 |
| Nkasi (Namanyele) | 2,422 | 2,355 | 2,319 |
| **Ruvuma (Songea)** | **2,403** | **2,308** | **2,256** |
| Mbinga | 2,416 | 2,320 | 2,289 |
| Namtumbo | 2,394 | 2,299 | 2,285 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 2,441 | 2,346 | 2,300 |
| Tunduru | 2,368 | 2,273 | 2,315 |
| **Shinyanga** | **2,365** | **2,297** | **2,261** |
| Kahama | 2,379 | 2,311 | 2,275 |
| Kishapu | 2,393 | 2,326 | 2,290 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 2,396 | 2,328 | 2,293 |
| Simiyu (Bariadi) | 2,406 | 2,339 | 2,303 |
| Busega (Nyashimo) | 2,399 | 2,332 | 2,296 |
| Itilima (Lagangabilili) | 2,409 | 2,342 | 2,306 |
| Maswa | 2,398 | 2,330 | 2,294 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 2,405 | 2,337 | 2,301 |
| **Singida** | **2,327** | **2,259** | **2,223** |
| Iramba | 2,339 | 2,271 | 2,235 |
| Manyoni | 2,311 | 2,243 | 2,208 |
| Ikungi | 2,322 | 2,255 | 2,219 |
| Mkalama (Nduguti) | 2,351 | 2,284 | 2,248 |
| **Songwe (Vwawa)** | **2,352** | **2,285** | **2,249** |
| Songwe (Mkwajuni) | 2,359 | 2,292 | 2,256 |
| Ileje | 2,356 | 2,289 | 2,253 |
| Momba (Chitete) | 2,361 | 2,294 | 2,258 |
| Tunduma | 2,356 | 2,289 | 2,253 |
| **Tabora** | **2,390** | **2,323** | **2,287** |
| Igunga | 2,344 | 2,276 | 2,241 |
| Kaliua | 2,409 | 2,342 | 2,306 |
| Ulyankulu | 2,403 | 2,336 | 2,300 |
| Nzega | 2,355 | 2,287 | 2,251 |
| Sikonge | 2,402 | 2,334 | 2,298 |
| Urambo | 2,403 | 2,336 | 2,300 |
| Uyui | 2,391 | 2,324 | 2,288 |
| **Tanga** | **2,300** | **2,203** | **2,066** |
| Handeni | 2,320 | 2,223 | 2,087 |
| Kilindi | 2,335 | 2,238 | 2,102 |
| Korogwe | 2,312 | 2,215 | 2,079 |
| Lushoto | 2,321 | 2,224 | 2,088 |
| Mkinga (Maramba) | 2,307 | 2,210 | 2,073 |
| Muheza | 2,304 | 2,207 | 2,071 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Pangani | 2,306 | 2,209 | 2,073 |

## JEDWALI B: BEI KIKOMO KWA BEI ZA JUMLA

| | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta ya Taa (Shs/Lita) |
|---|---|---|---|
| **DAR ES SALAAM** | **2,111.89** | **2,044.08** | **2,008.87** |
| **TANGA** | **2,175.36** | **2,078.33** | **1,943.21** |
| **MTWARA** | **2,193.14** | **2,097.91** | **-----** |

## JEDWALI C: SABABU ZA MABADILIKO YA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI

### BANDARI YA DAR ES SALAAM

| | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|
| **Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia** | Ongezeko la Dola 42.229/Tani | Ongezeko la Dola 30.094/Tani | Ongezeko la Dola 31.369/Tani |
| **Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (*BPS premiums*)** | Ongezeko la Dola 1.321/Tani | Punguzo la Dola 0.291/Tani | Punguzo la Dola 9.200/Tani |

### BANDARI YA TANGA

| | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|
| **Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia** | Ongezeko la Dola 42.229/Tani | Ongezeko la Dola 31.053/Tani | n/a |
| **Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (*BPS premiums*)** | Ongezeko la Dola 5.500/Tani | Ongezeko la Dola 5.500/Tani | n/a |

### BANDARI YA MTWARA

| | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|
| **Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia** | Ongezeko la Dola 42.229/Tani | Ongezeko la Dola 30.836/Tani | n/a |
| **Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (*BPS premiums*)** | Ongezeko la Dola 5.500/Tani | Ongezeko la Dola 5.500/Tani | n/a |

## JEDWALI D: BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA ZILIZOTUMIKA KUKOKOTOA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI

| | Bandari | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|---|
| **Mafuta yalipokelewa mwezi wa:** | **DSM** | Agosti 2019 | Agosti 2019 | Agosti 2019 |
| | **Tanga** | Agosti 2019 | Agosti 2019 | Julai 2019 |
| | **Mtwara** | Agosti 2019 | Agosti 2019 | n/a |
| **Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa mwezi:** | **DSM** | Julai 2019 | Julai 2019 | Julai 2019 |
| | **Tanga** | Julai 2019 | Julai 2019 | Juni 2019 |
| | **Mtwara** | Julai 2019 | Julai 2019 | ---- |

| | Bandari | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|---|
| **Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa miezi inayoonekana hapo juu inalinganishwa na wastani wa bei za mwezi:** | **DSM** | Juni 2019 | Juni 2019 | Juni 2019 |
| | **Tanga** | Juni 2019 | Juni 2019 | Juni 2019 |
| | **Mtwara** | Juni 2019 | Juni 2019 | ---- |

**Nzinyangwa E. Mchany**
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**
**EWURA**